JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KIGONIGONI

MWANGA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA

Shule ya Sekondari Kigonigoni

S.L.P 135,

MWANGA.

TAREHE……..

Namba za Simu;

Mkuu wa Shule; 0625203804

Makamu Mkuu wa Shule; 0620496531

Matron/Patron; 0620496531

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …….
……..
S.L.P ……..
…….

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KIGONIGONI HALMASHAURI YA MWANGA MKOA KILIMANJARO MWAKA …….**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka ……. na atasoma tahasusi ya ……

Shule ya Sekondari KIGONIGONI ipo umbali wa Kilometa 50 Mashariki mwa Mji wa MWANGA. Usafiri wa basi unapatikana kama ifuatavyo;

a) Kwa wanaotokea upande wa Arusha na Moshi basi linapatikana kituo kikuu cha mabasi cha moshi mjini. Kuanzia saa tatu asubuhi mpaka saa sita mchana kila

siku. Ulizia basi liitwalo Merenga ya Kigonigoni, nauli ni Tsh. **10,000/=** Toka Moshi mjini mpaka shuleni.

b) Kwa wanaotokea upande wa Dar es salaam, Tanga, Same shuka kituo kinachoitwa **lembeni** panda basi la **Merenga** kwenda kigonigoni ambalo linapatikana hapo kuanzia saa nane mpaka saa kumi jioni nauli Tsh. **5000/=** mpaka shuleni.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ……, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe …….. Mwisho wa kuripoti ni tarehe ……..(tarehe zingatia elekezi toka OR-TAMISEMI)

2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule ni suruali ya **KIJIVU ILIYOKOLEA (GREY DARK)** yenye marinda mawili mbele na isiwe yenye kubana (modal) zinatakiwa mbili upana nchi kumi na sita.
ii. Mashati mawili meupe ya mikono mirefu.
iii. Sare ya Michezo ni kaptula na fulana za rangi **NYEKUNDU**(T –shirt) zenye mistari miwili ubavuni (zisiwe na maandishi au nembo mfano chelsea au Barcelona). Na truck suti za rangi **NYEKUNDU** yenye mistari miwili meupe ubavuni
iv. Viatu vya shule ni **vyeusi** vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi (jozi mbili) **buti haziruhusiwi**.
v. Viatu vya michezo jozi moja kutegemea na mchezo anaoupendelea mwanao.
vi. Soksi jozi mbili nyeusi;
vii. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
viii. Sweta moja la rangi ya **kijivu**
ix. Nguo za kushindia ni flana ya rangi **NYEKUNDU,** shingo duara na isiwe na maandishi (isiwe jezi) na suruali **nyeusi** ya kitambaa yenye marinda mawili mbele upana wa miguu chini iwe 16
x. Tai **kijivu**ndefu (isiwe neck tie) kwa sare za shule.
xi. T- shirt ya shule zinapatikana shuleni kwa Tsh. 10,000/=

2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari 10 (3Q);
ii. **Ream (A4)** Mbili (2)
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*history 1 & 2, geography 1 & 2, english language 1& 2 kiswahili 1& 2)* vya TIE.
iv. Scientific Calculator kwa wanaosoma somo la jiografia
v. Godoro liwe size 2 ½ x 6
vi. Mashuka Jozi 2 ya **pink**, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 *nyeupe;*
vii. Nguo za ndani za kutosha;

viii. Vyombo vya chakula (kijiko, sahani/ bakuli lenye mfuniko, na kikombe viwe vya rangi nyekundu);

ix. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;

x. Vifaa vya usafi kwa mchanganuo ufuatao:

COMBINATION	VIFAA
HGK, HGLi	Jembe,kwanja1, toilet brush yenyempini wa plastik 1, mopper 1 mifagio 2 (soft broom 1 na chelewa1), sabuni ya maji lita tano ya chooni
HKL, HGFa	Panga,kwanja1, toilet brush yenyempini wa plastik 1, mopper 1 mifagio 2 (soft broom 1 na chelewa1), sabuni ya maji lita tano ya chooni
HGL	Kwanja,toilet brush yenyempini wa plastik 1, mopper 1 mifagio 2 (soft broom 1na chelewa1), sabuni ya maji 5 lita ya chooni

ANGALIZO: Vifaa vyote vinapatikana shule kwa bei sawa na mjini
Tunashauri ununulie shuleni ili kuepuka usumbufu wakati wa kusafiri n.k
kuhusu vifaa piga 0715501479.au 0620496531

2.3 Michango mbalimbali:

Mwanafunzi atakapo kuja ahakikishe amelipa michango elekezi kwenye jedwali hapo chini kupitia A/C No 40201100055 YENYE JINA LA KIGONIGONI SEKONDARI NMB BANK. ***Tanibihi hatupokei pesa mkononi wala kwa miamala ya simu tafadhali lipa Benki na uje na pay in slip.***

a) Shule za Bweni

Na	Aina ya Michango	Kiasi
1.	Mchango wa Uendeshaji wa Shule	65,000/=
3.	Tahadhari	5,000/=
4.	Nembo	5,000/=
5.	Kitambulisho cha Shule	5,000/=
	Jumla	**80,000/=**

b) Hakikisha umemkatia bima ya afya Mwanao ili aweze kupata huduma ya matibabu kwa urahisi tofauti na hapo utakuwa unalipia gharama za matibabu kila atakapougua.

3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku(Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

MUHIMU:

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na SIMU shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni haruhusiwi kutumia mawasiliano yeyote yale isipokuwa yaliyotolewa kwenye fomu hii, taarifa kutoka kwa mtu yeyote hata kama ni mtumishi wa shule hii haitapokelewa kwa kufanya hivyo hatua kali zitachukuliwa dhidi yake.**

3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

4. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII





MWL. STANLEY I. MGAYA

MKUU WA SHULE

A. FOMU YA UCHUNGUZI WA AFYA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI

NAMBA ZA SIMU

MKUU WA SHULE; 0625203804

MAKAMU MKUU WA SHULE; 0620496531

HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA

SHULE YA SEKONDARI KIGONIGONI

S. L. P. 135

MWANGA - KILIMANJARO

TAREHE: ……..

TO MEDICAL OFFICER
RE: …….
(Name of the student)
Pease examine the above named student as per medical examination form bellow.





STANLEY I. MGAYA
HEAD MASTER

MEDICAL EXAMINATION FORM
Full name:……..
Age:……..Height:……

1. Blood courting……..
2. Stool examination……..
3. Urine analysis……..
4. STDs……..
5. Leprosy test…….
6. Eye test…….
7. Chest……..
8. Abdomen ……..
9. Spleen ……

ADDITIONAL INFORMATION
E.g. physical defects or impairments, infections, chronic family diseases e.g. sickle cell……..
I ……i have examined the above mentioned student and therefore certify that he is FIT/ NOT FIT to pursue A level studies in your school.

SIGNATURE……. **WORKING STATION……**
DESIGNATION…… **DATE…….**

B. FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI NA MKATABA WAKUTOKUSHIRIKI MGOMO AU FUJO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA

SHULE YA SEKONDARI KIGONIGONI

S. L. P. 135

MWANGA - KILIMANJARO

TAREHE:……

MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

Mimi ……mwenye umri wa miaka…….mawasiliano ya wazazi au walenzi wangu ni kama ifuatavyo:

i. Ndugu …… wa S. L. P. …… mahali alipo……. Simu ya mkononi……..uhusiano wake na mwanafunzi…….

ii. Ndugu …… wa S. L. P. …… mahali alipo……. Simu ya mkononi……..uhusiano wake na mwanafunzi…….

MKATABA WA KUTOKUSHIRIKI MGOMO AU FUJO

Mimi ……..naahidi kuwa sintoshiriki wala kuhamasisha fujo au mgomo niwapo shuleni au nje ya shule. Nafahamu kuwa kufanya hivyo itakuwa kosa la kunifukuzisha shule. Pia naahidi kutii na kuzingatia sheria zote za shule. Na nchi yangu.

Saini ya mwanafunzi ……..Nimesaini leo tarehe ……
Mbele ya mzazi/mlezi wangu …….. saini ya mlezi/mzazi…….tarehe……..

C. FOMU YA MZAZI KUKIRI NA KUKUBALIANA NA SHERIA ZA SHULE NA MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA

SHULE YA SEKONDARI KIGONIGONI

S. L. P. 135

MWANGA - KILIMANJARO

TAREHE:……

UTHIBITISHO WA MZAZI

Mimi ……Mzazi/ Mlezi wa…… wa S. L. P. ……nimeyasoma masharti yote yanayohusiana na kijana wangu kujiunga na shule ya Sekondari Kigonigoni. Na **NIMEKUBALI/ SIJAKUBALI** (Kata isiyo sahihi) na kuahidi/ kukataa kuwa kijana wangu atafuata masharti yote ya shule. Nadhibitisha kuwa kijana wangu atatii walimu na wadau wengine wote katika elimu na malezi yake pindi awapo shuleni na hata nje ya shule.

NAKIRI KUWA NIMESOMA KANUNI ZOTE ZA SHULE NA TARATIBU ZAKE.

JINA LA MZAZI/……SAINI YA MZAZI……

TAREHE……

NAMBA YA SIMU…..

MWISHO

KARIBU SANA KIGONIGONI SEKONDARI

D. FOMU YA UTAMBUZI WA WAZAZI/WALEZI/NDUGU WATAKAOMTEMBELEA MWANAFUNZI

1



Jina .....

Uhusiano.....

Namba ya simu.....

2



Jina .....

Uhusiano.....
Namba ya simu.....

3



Jina .....

Uhusiano.....

Namba ya simu.....

4



Jina .....

Uhusiano.....

Namba ya simu.....

NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

- **Mkuu wa shule 0625203804**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0620496531**
- **Mwandamizi Taaluma 0712258722**
- **Mwandamizi Malezi 0715501479**